# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO - MASWALA YA JAMII

## KIPINDI CHA TANO:"NI UKWELI AU UONGO"

**MWANDISHI**: Chrispin Mwakideu
**MHARIRI**:Andrea Schmidt

**WAHUSIKA:** Eveline(19),Roni(14),Beti(12),Mkufunzi,Samu(14) Umati(Mseto), Mkuu wa sakafu

**Msimulizi**:

Hujambo na karibu katika kipindi cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu maswala ya jamii –jinsi ya kuwa kiongozi wa kisiasa. Katika kipindi kilichopita Eveline anayegombea udiwani katika uchaguzi wa serikali za mitaa, alizikataa pesa alizopewa na mbunge ili aachane na kampeni yake. Alifaulu kurekodi mazungumzo kati yake na mbunge huyo na hivyo kusaidia katika kumtia mbaroni kiongozi huyo. Dadake mdogo, Beti, alipitia mashindano makali katika uongozi wa kikundi chake cha uimbaji na kakake Roni akashauriwa na babake kuhusu mafunzo ya kucheza kandanda. Karibu msikilizaji katika kipindi chetu cha leo 'Je ni ukweli au ni uongo?'

**Onyesho la Kwanza: Nyumbani kwa Mapito. (chumba cha wasichana)**

**SFX: SAUTI ZA NDEGE NA JOGOO ANAWIKA**

(**Beti anaimba akisoma gazeti)**

**1.EVELINE:** Betty, tafadhali nyamaza.. bado nimelala

**2.BETTY:** Pole, dada.. nilikuwa nafanya mazoezi ya sauti yangu…

**SFX: SAUTI YA GAZETI LIKISOMWA**

**3.BETTY**: Eve! Eve!..Tazama picha yako wakati tukifanya usafi iko kwenye gazeti. Ngoja nikusomee maelezo yaliyoandikwa kukuhusu…

**4.EVELINE**: (**Apiga miyao**) huwezi kunisubiri nikaamka? Haya soma basi…

**5.BETTY**: Aha hii hapa. (**asoma kwa sauti ya juu**) "MWANASIASA CHIPUKIZI AMTIA MBUNGE KOROKORONI"

**6.EVELINE**: (**Shtuko**) Eti nini!!

**7.BETTY**: Hicho ni kichwa tu cha habari! Kuna zaidi (**aendelea**) Eveline mapito, diwani mtarajiwa wa kiti cha Milimani anafikiriwa kumtia mtegoni mjumbe kwa kuyanasa mazungumzo kati yake na yeye yaliopelekewa kukamatwa kwa mbunge huyo.. kwa madai ya hongo,ufisadi na maonevu…..

**8.EVELINE**: (**asema kwa mshangao)** Hebu lete**!**

**SFX: BETTY APOKONYWA GAZETI**

**8.EVELINE**: Mungu wangu! nimekwisha! Niliwaeleza waandishi wa habari ukweli wote na wamegeuza hadithi sasa ni mimi mwenye makosa? hakuna atakaye niamini tena…

**9.BETTY**: Usiseme hivyo.. sisi tunajua ukweli, tutakuamini..

**10.EVELINE**: La Beti, hunielewi.. nilikuwa niwe na kongamano leo na wakuu wa dini na wafanyabiashara ili wanichague kama mwanaharakati wao… watakaposoma haya hawataniamini….

**11.BETTY**: (**apumua kwa nguvu**) Pole, labda baba atakusaidia. Mimi nina mambo kemkem kuhusu kikundi changu..

**12.EVELINE**: Baba bado ana hasira na mimi.. lazima nijitafutie mbinu ya kujisafisha jina langu mwenyewe.

**13.BETTY**: Eve, jina lako halina uchafu wowote, wale walioandika hayo ndio wanafa kukusafishia jina lako na wakuombe radhi..

**14.EVELINE**: Swadakta Beti, maneno ya watu hayatauzuia mkutano wangu kamwe… Acha niendelee na kampeni zangu…

**15.MSIMULIZI.** Ni kweli kabisa wanayoyasema..mambo yanapokuwa magumu, wale walio mashujaa hujipa moyo na kuendelea kupambana. Baadaye siku hiyo hiyo Roni naye aliamua kuweka mbali majivuno yake na kurudi katika timu ya mpira ingawa hakuchaguliwa nahodha kama alivyotumai.

**<u>Onyesho la pili: katika uwanja wa mpira</u>**

**SFX: VIJANA WAKIKIMBIA KIWANJANI**

**1.KIJANA**: Lo!..Angalieni ni nani anakuja..

**2.VIJANA**: Ronnie! Ronnie! (**wanamuita jina lake)**

**3.SAMU**: Ala! Kwa hiyo umeamua kurudi? (**kejeli**) au ulitukosa?

Kwani sisi hatukukosa hata kidogo.. Tluifurahia kutokuja kwako…. tumekutoa timuni Roni…

**4.RONNIE**: Pole sana Samu! Ni mkufunzi pekee atakayenitoa kikundini sio wewe.

**5.SAMU**:( **ukakamavu)** Mimi ndio nahodha! na kama mkufunzi hayupo mimi hupitishwa maamuzi… na nimeamua…sikutaki katika timu yangu! ( **waanza kupigana na Roni amsukuma chini**)

**SFX: VIJANA WANAPIGA KELELE**

**6.MKUFUNZI**: Kunaendelea nini? heee Samu wewe ndio nahodha, hebu nieleze kwa nini mpira haupo hapa na kwanini… oh Roni pia wewe upo… na umepujuka… Usiniambie umerudi ili uanzishe vita?

**7.KIJANA**: (**wakimuogopa Samu**) Mkufunzi.. si Roni.. ni Samu… nahodha Samu ndiye aliyeanza kumpiga Roni…

**8.MKUFUNZI**: Eti ni kweli wavulana? Eti Samu ndiye aliyeanza haya yote?

**9.VIJANA**: Ndio mkufunzi!!!

**10.MKUFUNZI**: Samu, nilikupa uongozi wa kikosi hiki sio kwa kuwa ulikuwa bora kuliko Roni au wachezaji wengine. Nilifikiri utapata kuwajibika zaidi, ujifunze unyenyekevu na upate kujihusisha zaidi na mambo ya timu hii. Kumbe nilikosea.. ndio umekuwa katili, jangili, mkosa nidhamu mpaka wenzako wanakuogopa…ninakuvua wadhifa kama nahodha mpaka utakaponionyesha mabadiliko…

**11.SAMU**: (**ujeuri**) Aaaa thwuu! (**atema mate**) sijali… sikuwa na haja na uongozi wa timu ambayo kila siku inashindwa.

**12.RONNIE**: Samu…hayajaishia hapa.. nitakuripoti kwa mwalimu mkuu wa shule… baada ya mazoezi..

**13.MKUFUNZI**: Samu…Nataka uondoke mazoezini mara moja! Ondoka sasa hivi!!!

**14.SAMU: (anaenda akifoka)** Nendeni zenu!!! Siku zote mwashindwa tu!!!..

**15.MKUFUNZI**: Najuta kwa nini sikufanya haya mwanzoni.. Roni utakuwa nahodha ..unastahili.. chukua mpira na tuanze mazoezi …haraka vijana…

**SFX: KIPENGA KINALIA**

**16.MSIMULIZI**: Katika hali isiyo ya kawaida, Roni afanywa kuwa nahodha wa timu yake. Lakini katika mkutano wa viongozi wa kidini na wafanyabiashara, mambo yalikuwa moto moto kwa Eveline..

**<u>ONYESHO LA TATU: KATIKA UKUMBI WA JAMII</u>**

**MUZIKI UNASIKIKA**

**SFX: KELELE ZA WATU**

**1.MKUU WA SAKAFU**: Majaribio.. moja.. mbili… tatu…**(anasafisha koo)** chifu wetu, viongozi wa dini, wageni waalikwa, mabibi na mabwana….. karibuni katika mkutano ulioandaliwa na msichana wetu chipukizi, Eveline…

**2.UMATI**: (**kelele**) Mwongo! Mwongo! Mwongo!

**3.MKUU WA SAKAFU**: Tulieni tafhadhali! Tulieni1 Tusiugeuze mkutano huu kuw amaandamano. Tukumbuke kuwa katiba yetu inasema mtu hana hatia mpaka korti imhukumu … yale tuliyoyasoma leo bado yanachunguzwa… Ni furaha yangu kumkaribisha Eveline Mapito awahutubie..

**SFX: Sauti za kumsifu na kumkejeli**

**4.EVELINE**: Asanteni kwanza kwa kuniruhusu kuwahutubia…watu wengi wananiuliza na udogo huu nitaiwezaje siasa? Jibu langu ni lile lile..siasa sio umri, bali ni kuboresha maisha ya wale unaowaongoza..Ni kujitolea kuyaweka masilahi yao mbele ya masilahi ya kibinafsi. Hii ndio sababu nagombea udiwani wa Milimani…

**SFX: MAKOFI MACHACHE**

Nimewaita hapa kuwaomba msaada wenu..na kura zenu na pia kuwahakikishia kwamba nikichaguliwa, naahidi kumtumikia kila mtu sawa sawa pasipo kujali kabila, dini, jinsia, umri au tabaka la kijamii. Nitapambana na ufisadi na ubadhirifu wa raslimali za umma kuanzia siku ya kwanza nitakayochaguliwa.

**SFX: MAKOFI MENGI**

**5.MWANAHABARI**: Kunradhi, mimi ndiye mwanahabari..aliyekuhoji wakati wa zoezi la kusafisha jiji. Najua watu wana hamu kubwa kusikia ukweli. Je ni kweli au uongo kwamba ulimtega mbunge wako kushitakiwa kwa makosa ya ufisadi ili uwe mgombea maarufu wa kiti cha udiwani?

**6.SFX: KELELE ZA WATU NUN'GUNIKO**

**7.EVELINE**: Natamani ningeweza kujibu hayo hapa hadharani lakini sheria hainiruhusu… kesi bado inaednelea na mambo hayo yatatatuliwa mahakamani…Ninachoweza kukisema ni…nihukumu kwa yale niyafanyayo lakini sio kwa yale yanayoandikwa na magazeti. Unatakiwa ufahamu kwamba gazeti lilichochapisha ripoti hii linamilikiwa na mbunge mwenyewe na tayari wamenipigia simu kuniomba radhi

**8. CROWD**: (**Shangwe na nderemo**) EVELINE! EVELINE!

**MWISHO WA KIPINDI CHA TANO**

**<u>Msimulizi</u>**

Kwa hivyo msikilizaji jukwaa limeshaandaliwa kwa mashindano makali ya kuwania udiwani wa eneo la Milimani. Jiunge nasi wiki ijayo ujifunze ikiwa kila mtu anajua kufuata sheria. Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe Hadi mara nyingine kwaheri!